

**A Ni nani aliye huru? Warumi 8:1.**

- ❖ Ni wale tu walionauhusiano imara na Kristo wanaweza kuwa huru; hiyo hujumuisha muungano uliochangamka wa kila siku pamoja Naye.

**B Tunawekwa huru dhidi ya nini? Warumi 8:2.**

- ❖ Tofauti na sheria ya dhambi, sheria ya Roho huleta uhuru na uzima. Sheria ya dhambi huleta mauti na hukumu ya milele pekee.

**C Tunawezaje kuupata Uhuru? Warumi 8:3.**

- ❖ Sio kwa sheria, kwa sababu ina uwezo wa kutuhumu tu, kwani tu wadhambi.
- ❖ Kupitia maisha na kifo cha Kristo aliyekuwa mwili na kuishi bila dhambi.

**D Tuishije baada ya kuwekwa huru? Warumi 8:4.**

- ❖ Hatutawaliwi tena na tamaa zetu wenyewe, lakini kwa amri na uongozi wa Roho Mtakatifu anaeishi ndani yetu.
- ❖ Kwa hiyo, kuenenda kwa Roho humaanisha kuishi kulingana na matakwa ya sheria: maisha ya upendo na utii wa upendo.

**E Twawezaje kutambua kama tunaishi kulingana na Roho au mwili (Warumi 8:5-8)? Warumi 8:5-8.**

- ❖ KUISHI KULINGANA NA MWILI.
  - Kufikiri na kufanya vitu vya mwili.
  - Matokeo yake ni dhambi.
  - Kukosana na Mungu na kushindwa kumpendeza.
  - Kushindwa kuitii sheria ya Mungu.
- ❖ KUISHI KULINGANA NA ROHO
  - Kufanya na kufikiri juu ya vitu vya Roho.
  - Matokeo yake ni Amani na uzima.
  - Kuwa mwana wa Mungu na kuishi ukimpendeza.
  - Hujisalimisha kwa sheria ya Mungu.

**F Tunawezaje kuishi tukifikiri mambo ya kiroho? Warumi 8:9-14.**

- ❖ Tunakuwa wakiroho pale tunapoongozwa na kuvutwa na Roho Mtakatifu, kwa kumruhusu Yeye kukaa ndani yetu.
- ❖ Roho anaishi ndani yetu panapokuwa na uhusiano wa karibu kati ya Roho na sisi. Hiyo huhusisha kila mara kujisalimisha kwa mapenzi ya Mungu. Roho ana nguvu kubadilisha maisha yetu.

**G Je; yapi ni matokeo ya kuishi kwa kufuata Roho? Warumi 8:15-17.**

- ❖ Sasa:
  - Tuko huru dhidi ya hofu kwa sababu dhambi zetu zimesamehewa.
  - Tunafanywa kama watoto wa Mungu.
  - Mungu ni baba yetu na anatutunza.
  - Ni warithi wa Mungu kwa sababu sisi ni watoto wake.
  - Yesu hushiriki urithi wake pamoja nasi.
  - Tunateseka pamoja na Kristo.
- ❖ Baadaye:
  - Tutarithi ufalme wa utukufu na uzima wa milele.
  - Tutatukuzwa pamoja na Kristo.